# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA NANE

**18 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA NANE - TAREHE 18 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**613 MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini uhakiki wa Wastaafu utafanyika Wilayani badala ya Mkoani kama ilivyo sasa ili kuwaondolea usumbufu wa kusafiri umbali mrefu.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**614 MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Mwabuzo - Meatu kuwa Kituo cha Afya.

**615 MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Watoto wenye Mahitaji Maalum katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini.

**616 MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha kukarabati na kujenga madarasa mapya katika Shule kongwe ili kuboresha mazingira ya kujifunzia.

**617 MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba chini ya Mpango wa TACTIC.

## WIZARA YA KILIMO:

**618 MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, hekta ngapi zinafaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji katika Mkoa wa Mtwara.

## WIZARA YA UJENZI:

**619 MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Ujenzi wa Barabara ya TAMCO - Mapinga kwa kiwango cha lami utakamilika kwani imekuwa ikijengwa vipande tangu mwaka 2018.

## WIZARA YA MAJI:

**620 MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga Mradi wa Maji kupitia Benki ya Dunia Kata za Murray, Nambis, Kainam, Nahasey na maeneo jirani Tarafa ya Nambis.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**621 MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali itatunga Sheria itakayomshurutisha Mtoto kuwatunza Wazazi wake wakizeeka.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**622 MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Wananchi wa Mafia watapata usafiri wa uhakika wa njia ya maji.

**623 MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Bandari ya Dar es Salaam iliyoboreshwa itaanza kusafirisha Mazao ya Mbogamboga, Mifugo na Matunda.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**624 MHESHIMIWA SEIF SAID KHAMIS GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu Vijiji vya Uswaya, Ncheli, Mwakabuta na Mpogolo - Manonga.

**625 MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka minara ya simu maeneo ya Kata ya Mwema, Nyansicha na Itiryo - Tarime Vijijini.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **18 JUNI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA